# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA KUMI NA MBILI

**14 FEBRUARI, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

### KIKAO CHA KUMI NA MBILI – TAREHE 14 FEBRUARI, 2024

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**192. MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, kwa nini Serikali isifanye utaratibu wa kwenda kuhakiki Wastaafu kwenye Wilaya zao kuliko ilivyo sasa kuhakikiwa Mikoani.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**193. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa upungufu wa Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari nchini.

**194. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa Shule ya Sayansi ya Wasichana Mkoani Katavi.

**195. MHESHIMIWA STANSLAUS SHING'OMA MABULA (NYAMAGANA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha mchakato wa kuanzisha Tarafa za Igoma na Mkolani - Nyamagana.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**196. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali inafanya nini kuhakikisha Miradi ya TASAF inakuwa yenye tija kwa Wanufaika.

**WIZARA YA KILIMO:**

**197. MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU (TUNDURU KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji katika Kijiji cha Nambalapi Kata ya Masonya - Tunduru utaanza.

**198. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (ULYANKULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, bei ya mfuko wa mbolea itakuwa Shilingi ngapi baada ya Serikali kuweka ruzuku nchi nzima.

**199. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (NSIMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Mradi wa Umwagiliaji katika Kata ya Urulwa Kijiji cha Usense - Nsimbo.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**200. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya viwanja vilivyouzwa na Halmashauri ya Wilaya Kibaha eneo la Kisabi na baadae kuzuiwa kuviendeleza.

**201. MHESHIMIWA ALEKSIA ASIA KAMGUNA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali imejipangaje kukomesha migogoro kati ya Wakulima na Wafugaji.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**202. MHESHIMIWA MUSTAFA MWINYIKONDO RAJAB (DIMANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itamalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi Maungani – Dimani kilichojengwa kwa nguvu za Wananchi.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**203. MHESHIMIWA JUSTIN LAZARO NYAMOGA (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itafunga mitambo ili Wananchi wa Tarafa ya Kilolo wapate matangazo ya Redio ya Taifa (TBC).

**WIZARA YA MAJI:**

**204. MHESHIMIWA TECLA MOHAMED UNGELE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Wananchi wa Kata za Nachingwea, Kiegei, Matekwe, Namapwia – Nachingwea na Lihimalya, Kandawale – Kilwa watapatiwa maji.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**205. MHESHIMIWA AMINA ALI MZEE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia ajira ya kudumu Vijana ambao wanatumiwa kama vibarua kwenye ujenzi wa Reli nchini.

**206. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI (TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mkakati gani kumaliza migogoro kati ya Bajaji na Daladala katika Miji mingi nchini inayotokana na *routes* kugongana.

**WIZARA YA UJENZI:**

**207. MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MASWA MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa barabara kutoka Njiapanda/Ikungu kwenda Malampaka kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA NISHATI:**

**208. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE JUMBE MLAGHILA (KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini ujenzi wa Kituo cha Umeme *(Substation)* utaanza - Kyela.

**WIZARA YA FEDHA:**

**209. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzisaidia *Community Banks* kama MUCOBA Bank Iringa ili kukuza uchumi wa Wananchi wa hali ya chini.

**WIZARA YA AFYA:**

**210. MHESHIMIWA ESTHER LUKAGO MIDIMU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itajenga uzio katika Hospitali ya Mkoa wa Simiyu.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (*PIC*):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**DODOMA**
**14 FEBRUARI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**